**SIGNAL SPARKS PREDICTION TEST 1**
**Kenya Certificate of Primary Education**

# — KISWAHILI—

**504**

SIGNAL Publishers
Igniting thinking

## SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA

**JUNE. 2022 - Muda: Saa 1 dakika 40**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA(Soma maagizo yafuatayo kwa makini)**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.

2. Ukiisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba karatasi ya majibu uliyopewa imejumuisha yafuatayo.
   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

5. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
6. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.

7. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.

8. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.
   **Mfano**
   **Katika kijitabu cha maswali:**

**21. Kamilisha kwa neno lifaalo zaidi**. Kaka aliniandikia _______ ya kulipa karo shuleni.

A. hawara
B. awala
C. hawala
D. awara

Jibu sahihi ni C (**hawala**)

**1.** [A] [B] [C] [D] **11.** [A] [B] [C] [D] **21.** [A] [B] [C] [D] **31.** [A] [B] [C] [D] **41.** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 21, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

9. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako **kiwe cheusi** na kisijitokeze nje ya kisanduku.
10. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa**

SIGNAL Publishers
Igniting thinking

©*Signal Publishers Limited 2022*

**Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Lugha ya binadamu yeyote __1__ na mazingira __2__. Mathalani, mtoto __3__ na wazazi ambao shughuli zao kuu ni kilimo, __4__ msamiati atakaotumia utahusiana na __5__. Utamsikia kwa mfano akitaja __6__ ambao ni msimu wa mvua nyingi. Mtoto yuyo huyo __7__ kuvaa mavazi yanayovaliwa na wale jamaa wakubwa walio karibu naye kwani __8__.

1. A. huathirika B. huathiriwa C. huathiriana D. huathirikia
2. A. yako B. yao C. yenu D. yake
3. A. angelelewa B. analelewa C. akilelewa D. akalelewa
4. A. baadhi ya B. mithili ya C. kati ya D. fauka ya
5. A. zaraa B. sanaa C. zinaa D.bidhaa
6. A. vuli B. kifuku C. chaka D. kipupwe
7. A. atapendeza B. atapendekeza C. atapendea D. atapendelea
8. A. mwana mui ni dawa ya mlango B. damu ni nzito kuliko maji C. mtoto akibebwa hutazama kisogo cha nina D. badiliko kwa mjukuu uanze na babu

Mapenzi yangu kwa somo la Kiswahili __9__ nijifunze kwa __10__ kuu. Nakumbuka __11__ kwa kutambua idadi ya silabi katika maneno. Kwa mfano, neno mkokoteni lina silabi __12__. Pia nilipenda kutumia vivumishi kama vile __13__ kufafanulia zaidi kuhusu nomino mbalimbali. Niliweza hata kutambua sentensi zenye masharti, kwa mfano __14__. Hata nilipohitimu masomo ya darasa la nane, haikuwa vigumu kutunga mashairi ya __15__ ambayo huwa na mishororo mitatu katika kila ubeti.

9. A. lilinifanya B. kilinifanya C. yalinifanya D. ilinifanya
10. A. ari B. shaka C. dhima D. dhana
11. A. nilipoanza B. nilikoanza C. niliyeanza D. nilivyoanza
12. A. 4 B. 3 C. 5 D. 9
13. A. safi, kali, sana B. bora, gani, kadha C. tele, zaidi, bora D. vile, kando, zao
14. A. kihifadhi mahali salama B. ukifika mapema unijulishe C. kile kitatunzwa na mwenyewe D. walikuwa wakienda mjini
15. A. tathlitha B. takhmisa C. tasdisa D. tathnia

**_Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu sahihi._**

16. Chagua sentensi yenye nomino fungamano.
 A. Sitausahau wema alionitendea.
 B. Maziwa huwasaidia watoto kuwa wenye afya.
 C. Batamzinga ni ndege wa kuvutia sana.
 D. Taifa la Kenya lina raia wengi.

17. Njuga ni kwa mguu na _______ ni kwa pua.
 A. kikuku
 B. furungu
 C. jebu
 D. kishaufu

18. Chagua nahau yenye maana sawa na **'kula mwata'**.
 A. Kula mumbi
 B. Kula mwande
 C. Kula njama
 D. Kula nyara.

19. **Andika wingi wa sentensi ifuatayo.**
 Jirani yangu alihamia shambani alipougua kifuakikuu.
 A. Majirani zangu walihamia mashambani walipougua vifua vikuu.
 B. Jirani yetu alihamia mashambani alipougua kifuakikuu.
 C. Majirani zetu walihamia mashambani walipougua kifuakikuu.
 D. Majirani wetu walihamia mashambani walipougua vifua vikuu.

20. **Upi ni muungano sahihi wa sentensi zifuatazo?**
 Panya aliingia darasani. Panya aliwatatiza wanafunzi.
 A. Panya aliingia darasani lakini aliwatatiza wanafunzi.
 B. Panya aliingia darasani akawatatiza wanafunzi.
 C. Panya aliingia darasani akiwatatiza wanafunzi.
 D. Panya angeingia darasani angewatatiza wanafunzi.

21. Chagua sentensi yenye kiwakilishi cha idadi.
 A. Vijana wengi walishiriki uchaguzi huo.
 B. Yule atawakaribisha wageni wawili.
 C. Wao waliongozana hadi shuleni.
 D. Vingi vinaletwa na wenyeji wa mji huo.

22. Vifaa vipi hutumika katika uhunzi?
 A. Mvuo na fuawe.
 B. Timazi na msasa.
 C. Koleo na kwanja.
 D. Utepe na kumbwewe.

23. **Kanusha sentensi ifuatayo.**
 Vibarua wanavuna mahindi wakiyatia ghalani.
 A. Vibarua hawakuyavuna mahindi wala kuyatia ghalani.
 B. Vibarua hawavuni mahindi wakiyatia ghalani.
 C. Vibarua hawajavuna mahindi wakayatia ghalani.
 D. Vibarua hawatavuna mahindi wala kuyatia ghalani.

24. **Tegua kitendawili kifuatacho.**
 Useja wangu mrefu lakini hauvaliki shingoni.
 A. Moshi
 B. Kamba
 C. Kivuli
 D. Siafu.

25. Neno lipi lina silabi yenye herufi mwambatano?
 A. Manufaa
 B. Kiota
 C. Mbung'o
 D. Mkeka.

26. **Udi** ni magome ya mti yanayotoa harufu nzuri yanapoungua. **Udi** pia ni
 A. ala ya muziki
 B. tenda jambo la kuleta kero
 C. upanga wa jogoo
 D. uzi wa usumba wa nazi.

27. **Andika usemi wa taarifa wa sentensi ifuatayo.**
 Mwaye: Mwanangu, nitakupeleka zahanatini kesho.
 A. Mwaye anamwambia mwanawe kuwa atampeleka zahanatini.
 B. Mwaye alimwambia mwanawe kuwa angempeleka zahanatini kesho.
 C. Mwaye alimwambia mwanawe kuwa atampeleka zahanatini siku ambayo ingefuata.
 D. Mwaye alimwambia mwanawe kwamba angempeleka zahanatini siku ambayo ingefuata.

28. **Sahau** ni kwa **usahaulifu** kama vile **legea** ni kwa
 A. legevu
 B. ulegevu
 C. legeza
 D. mlegevu.

29. Akisami $^7/_8$ kwa maneno huitwa
 A. subui nane
 B. thumni saba
 C. humusi saba
 D. humusi nane.

30. **Chagua methali yenye maana sawa na hii.**
 Mtu hujikuna ajipatapo.
 A. Kila chombo na wimbile.
 B. Bidii ya mja haiondoi kudura.
 C. Kila chungu na tamule.
 D. Mtu huenda na uchao haendi na uchwao.

**Geuza ukurasa**

**_Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 31 mpaka 40._**

Utamaduni ni jinsi binadamu anavyokabili maisha katika mazingira yake. Hiyo inajumuisha ujuzi, imani, sanaa, maadili, sheria, desturi na kadhalika ambavyo mtu anajipatia kama mwanajamii. Bila shaka, utamaduni ni sifa maalum inayomtofautisha binadamu na wanyama. Ni muhali kwa mnyama kuwazia utamaduni seuze kuwa na utamaduni wao wenyewe? Kwa hivyo, tunaweza kudai kuwa utamaduni ndio humjengea binadamu utu.

Katika jamii mbalimbali, utamaduni hurithishwa kupitia mafunzo mbalimbali ambapo mengi hupitishwa kwa njia ya mdomo. Mbinu maarufu zaidi katika kupitisha utamaduni ni ngano, nyimbo, methali, vitendawili, misemo na maigizo. Nchini mwetu huwemo siku mahsusi ya utamaduni ambayo huadhimishwa kitaifa. Katika siku hii, wazee hujivunia utamaduni wao huku vijana wakijielimisha kuhusu masuala mbalimbali yanayozingatiwa na jamii zao.

Hebu fikiria jinsi ulivyokuja kujua nini cha kuliwa, mavazi, lugha na shughuli zako za kila siku. Je, ulifunzwa shuleni? Bila shaka jibu la swali hili unalijua. Tujuavyo, **mwana akibebwa hutazama kisogo cha nina**. Vivyo hivyo, ndivyo ulivyojifunza mambo muhimu kutokana na utamaduni wa wanajamii wenzako.

Watu wenye utamaduni sawa hujihisi kama familia moja. Wao hutenda mambo yao kwa kikoa. Huona raha wanapojitambulisha kupitia lugha yao, nyimbo zao, mapishi yao na hata shughuli zao za kiuchumi kama vile kilimo, uvuvi, ufugaji, uwindaji na usukaji. Mmoja amwonapo mwenzake, hupata mvuto wa kuwa karibu na ndugu. Haikosi utawaona wakisalimiana kwa lugha yao huku wakicheka kwa furaha. Hebu kumbuka siku ulipokutana na mtu wa jamii yako katika sehemu ya mbali na kwenu. Labda utaniambia kuwa ulimkimbilia, ukamkumbatia na kumpiga pambaja kwa mahaba. Naam, huo ndio utamaduni hasa, ndio uzi uliokuvuta pamoja na mwenzako huyo.

Utamaduni wa jamii huandamana na namna ya **miiko**. Wanajamii hutahadharishwa dhidi ya vitendo fulanifulani ambavyo vinaweza kuwaletea madhara. Uvunjaji wa miiko hii hufungamanishwa na adhabu kama vile kupigwa radi, ajali, kichaa na nyingine kalikali. Miiko hii huimarisha utunzaji wa mazingira, heshima baina ya wazee na vijana, mahusiano kati ya vijana na wenzao, kuheshimu mali ya wengine miongoni mwa mambo mengine mengi. Bila mpangilio mwafaka uletwao na utamaduni, maisha ya binadamu yangevurugika mchafukoge.

Ni muhimu kuelewa kwamba utamaduni ni kitu kinachokua kila siku. Utamaduni humtia binadamu kiu ya kupata maarifa mapya na kubadilisha maisha yake kwa njia iliyo bora zaidi. Hii ina maana kuwa binadamu, kupitia wanazuoni, ana nafasi ya kuchunguza mtindo wake wa maisha, aepuke mambo yasiyofaa maishani. Haya ni pamoja na ukeketaji, ndoa za mapema na urithi wa wajane. Mambo haya hutushushia hadhi yetu. Tunapaswa kuyakumbatia mambo yanayoongeza thamani maishani mwetu.

Sisi vijana hatuna budi kuukumbatia utamaduni wetu. Utamaduni ni baba na mama. Ni nani anayeweza kumkana mvyele kadamnasi. Tusipumbazwe na utamaduni wa kigeni tunaojifunza kwenye runinga na mitandao ya kijamii. Baadhi ya mambo tunayojionea pale yanaweza **kututia kisimani**. Waama, mwacha mila ni mtumwa.

**31.** Aya ya kwanza inasema kuwa

A. utamaduni wa wanyama ni tofauti na wa binadamu

B. wanyama hujifunza utamaduni kutoka kwa binadamu

C. uelewa wa binadamu ndio humwezesha kuwa na utamaduni

D. utamaduni wa binadamu hutegemea watakavyoishi wengine.

**32.** Siku ya utamaduni ni muhimu kwa yote haya ila

A. vijana hupitisha utamaduni kwa vizazi

B. wazee hufurahia utamaduni wao

C. vijana hupata mafunzo kuambatana na utamaduni

D. ni njia mojawapo ya kuliunganisha taifa.

**33.** Methali '**<u>Mwana akibebwa hutazama kisogo cha nina</u>**' jinsi ilivyotumika ina maana kuwa

A. mtoto hujifunza utamaduni kutoka kwa mama yake

B. mtindo wa mtoto wa maisha huathiriwa na wale anaoishi nao

C. shughuli za kila siku hutegemea yale anayofunzwa mtoto shuleni

D. mtoto abebwapo mgongoni hukitazama kichwa cha mama yake.

**34.** Watu wakiwa na utamaduni sawa

A. hufahamikiana na kucheka pamoja

B. hutambua shughuli zao na kukutana zaidi

C. hujivunia utamaduni na kuishi karibu karibu

D. huimarisha uhusiano na kushirikiana zaidi.

**35.** Jambo lipi halihusiani na utamaduni kwa mujibu wa kifungu?

A. Mavazi

B. Chakula

C. Ukoo

D. Sanaa.

**36.** Mwandishi wa makala haya

A. ana uhakika kuwa msomaji huwakumbatia watu wa jamii yake

B. alimkumbatia mwenzake kwa mahaba walipokutana na kujuana

C. anaona kuwa inawezekana msomaji alifurahi alipokutana na mtu mwenye utamaduni kama wake

D. anathamini sana mambo ya utamaduni wa watu wakutanao mbali na kwao.

**37.** Umuhimu wa miiko kulingana na kifungu ni

A. kudhibiti tabia za watu katika jamii

B. kuonya watu dhidi ya mikasa katika jamii

C. kuwaadhibu wanaokiuka kaida katika jamii

D. kumulika mienendo ya vijana katika jamii.

**38.** Aya ya sita imeonyesha dhahiri shahiri kuwa

A. si vizuri kuacha lolote linalohusiana na utamaduni wetu

B. utamaduni unapaswa kubadilika kwa njia inayoongeza thamani maishani

C. mambo mengi ya kitamaduni tunayozingatia yamepitwa na wakati

D. tunapaswa kuyakumbatia mambo mapya siku zote.

**39.** "**<u>Ni nani anayeweza kumkana mvyele kadamnasi?</u>**"

Kauli hii inatukumbusha kuwa

A. tusiwakaidi wazazi wetu mahali popote

B. ugomvi wa watoto na wazazi usifanyike hadharani

C. baba na mama ni muhimu kuliko utamaduni

D. tusivutiwe na miigo tuhasi utamaduni wetu.

**40.** Maana ya '**<u>kututia kisimani</u>**' kulingana na muktadha ni

A. kutupotosha

B. kutukosoa

C. kutuvuruga

D. kutuua.

**Geuza ukurasa**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 41 mpaka 50**

Wanyama walitatizika kwa muda. Hawakuwa na yeyote wa kuwatatulia matatizo yao. Walipofanya mkutano, iliishia kuwa yenye rabsha kochokocho. Hii ilikuwa ni baada ya kifo cha mfalme wao Simba. Hali ilipokithiri, wale wenye nguvu walianza kuwaangamiza wenzao bila hisia zozote. Hawakuhofu lolote kwani hapakuwa na yeyote wa kuwachukulia hatua dhidi ya vitendo vyao. Ama kweli, nchi yao ilibadilika kuwa ulimwengu wa mnyonge msongeni.

Ni katika hali hii ambapo kamati ya wanachama saba ilichaguliwa ili kulishughulikia suala la uongozi. Hawa walikuwa Fisi, Sungura, Nyati, Mamba, Buibui, Chatu na Nyani. Kamati hii ilizunguka kote ikikusanya maoni kutoka kwa wanyama wengine. Matokeo ya utafiti yalionyesha wazi kuwa wanyama walihitaji kuwa na kiongozi ambaye angeliokoa jahazi lao lisizame! awaletee ustawi kama ule ulioshuhudiwa wakati wa Simba.

Vikao zaidi viliandaliwa, hatimaye wanyama wale wakampendekeza Fisi awe kiongozi wao. Fisi alitabasamu na kuchekacheka kama ilivyokuwa ada yake. Alihofia kuwa ile hulka yake ya kutamani vya bure ingemchongea na kuutia doa utawala wake. Hata hivyo, alijikumbusha kwamba, akiwa mfalme, angekuwa na kila kitu. Kwa hivyo, hapakuwa na hofu ya kutamani zaidi kwani asingekosa chochote. Hata hivyo, ili kuficha fikira zake kwa wengine, alijitia kuwaza kidogo akasema, "Ndugu zangu, wadhifa wa ufalme ni mkubwa sana. Kama tujuavyo, kichwa cha kuku hakistahimili kilemba. Naomba mfikirie sana kabla ya kunitwika jukumu hili". **Kimoyomoyo, fisi alijilaani kwa kuyatamka maneno haya**. Alihofia yasije kumnyima nafasi hii ya kipekee.

Baada ya ushawishi wa wanyama, Fisi alikubali kuyatwaa mamlaka. Awali, alikuwa kiongozi bora sana. Wanyama wakavutiwa na utawala wake. Wengine walisikika wakisema kwamba Fisi aliinukia kuwa kiongozi bora kuliko mtangulizi wake. Alimiminiwa sifa kemkemu kutoka karibu na mbali.

Ama kwa hakika, tabia ni kia cha mwili. Ile **hulka ya Fisi ya kutotosheka ilimnyemelea tena na kumkumbatia ghafla**. Alianza kutoa maagizo na hata maamuzi yaliyomfaidi yeye binafsi. Mathalani, wale waliomwendea wakiwa na migogoro kuhusu umiliki wa mali, alizitwaa mali hizo na kuzifanya zake binafsi. Isitoshe, alianza kuwatoza wanyama kodi kubwa kutokana na mapato yao. Yote haya alisema yalikusudia kuleta maendeleo ya haraka katika himaya yao. Wanyama walitii maagizo haya kwa kuchelea kuangamizwa na walinzi wa mfalme ambao walikuwa waaminifu kwake siku zote.

Siku moja, Fisi aliamkia maasi makubwa katika ufalme wake. Wanyama walikuwa wamefikwa kooni na ukatili wa kiongozi wao. Walinzi walijaribu kusimama kidete. Fisi naye aliamua kuitetea hadhi yake. Akaamua kupigana kufa kupona. Lakini tujuavyo, maji mengi hayazuiliki. Fisi na walinzi wake walilazimika kuchana mbuga kunusuru roho zao.

Teacher.co.ke

41. Matatizo ya wanyama yalichangiwa zaidi na
   A. hali mbaya ya anga katika eneo hilo
   B. ukosefu wa utawala wa kuangazia shida zao
   C. kujiuzulu kwa mfalme wao wa zamani
   D. uongozi mbaya wa wanyama wenye nguvu.

42. Umuhimu wa kiongozi kulingana na makala haya ni
   A. kushughulikia maslahi ya wanajamii, kuwachukulia hatua wanaokiuka sheria
   B. kuzuia majanga katika jamii, kuwapiga jeki wanaowadhulumu wenzao
   C. kuwatetea wale wasio na uwezo mkubwa katika jamii
   D. kuunganisha jamii na kupinga wanaoenda kinyume na utawala wao.

43. Kamati ilifanya kazi kwa uadilifu kwani
   A. iliundwa kwa wanyama wa jamii zote porini
   B. iliongozwa vyema chini ya usimamizi wa Sungura
   C. iliwahoji wote waliotaka nafasi ya kuongoza
   D. iliwahusisha watawaliwa katika uamuzi kuhusu uongozi.

44. Ni wazi kuwa
   A. Simba hakua kiongozi mwadilifu
   B. utawala ulidhoofika wakati wa uongozi wa Simba
   C. Simba alikuwa ameleta maendeleo ya kuridhisha
   D. wanyama walisafiria jahazi lililoelekea kuzama.

45. Yaelekea kuwa waliompendekeza Fisi kuwa kiongozi ni
   A. marafiki zake
   B. wanakamati
   C. wenye nia mbaya
   D. wanadamu.

46. '<u>Kimoyomoyo, Fisi alijilaani kwa kuyatamka maneno haya.</u>' Kifungu hiki cha maneno kinaonyesha kuwa Fisi
   A. anashuku kuwa huenda akashindwa kuongoza
   B. anawalaumu wale wanaodai hawezi kuongoza.
   C. ana uhakika kwamba hatakuwa kiongozi bora.
   D. anajutia matamshi yake ya kukataa uongozi.

47. Kifungu kimedhihirisha kwamba
   A. awali, Fisi alijaribu kuyaepuka mazoea yake yasiyofaa
   B. tangu mwanzo, Fisi alidhihirisha tabia yake ya ubinafsi
   C. Fisi alileta maendeleo makubwa hata kuliko Simba
   D. mtangulizi wa Fisi hakuwa kiongozi bora kwamwe.

48. Lengo la Fisi katika kuwatoza wanyama kodi kubwa lilikuwa
   A. kuwaadhibu
   B. kuleta maendeleo
   C. kujifaidi
   D. halijulikani.

49. "<u>Hulka ya Fisi ya kutotosheka ilimnyemelea tena na kumkumbatia ghafla.</u>" Maneno haya yametumia tamathali gani ya usemi?
   A. Tashbihi
   B. Tashhisi
   C. Sitiari
   D. Ishara.

50. Kichwa kifaacho zaidi kwa makala haya ni
   A. Njia ya mwongo ni fupi.
   B. Ukubwa ni jaa.
   C. Mwenye pupa hadiriki kula tamu.
   D. Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani.

**Geuza ukurasa**